**Learning on TAP**




# Teknolojia saidizi

Jumbe muhimu: Vifaa saidizi vya usikivu

## Somo 1: Usikivu na matatizo mbalimbali ya usikivu

### Usikivu ni nini?

Usikivu ni uwezo wa kutambua na kuelewa sauti katika mazingira. Masikio hukusanya mitetemo ya sauti na kuwa mithili ya umeme ambao husafiri hadi kwenye ubongo. Miali hii ya umeme ikifika kwenye ubongo, huwa tunasikia na kuitambua. Ili kusikia vizuri, ni lazima sehemu zote za sikio ziwe na afya njema na zifanye kazi ipasavyo. Sehemu tofauti za sikio zinazohusika kwenye kusikia:

| Sehemu ya sikio | Jukumu | Mambo muhimu | Picha |
|---|---|---|---|
| Sehemu ya nje ya sikio | Hukusanya sauti kutoka hewani na kuielekeza kwenye mfereji wa sikio | Nnta yenye rangi ya njano au kahawia inazalishwa kwenye mfereji wa sikio. Nnta husaidia kulinda sikio na kulisafisha. Kwa kawaida uchafu hutoka wenyewe kupitia mfereji wa sikio |  |
| Sehemu ya kati ya sikio | Huongeza ukubwa wa sauti | Mfereji wa sikio uelekea kwenye ngoma ya sikio ( utando wa timpaniki) Ngoma ya sikio inatofautisha mfereji wa sikio na sehemu ya ndani ya sikio |  |
| Sehemu ya ndani ya sikio | Inabadilisha sauti kwenda kwenye miali ya umeme | Sehemu ya ndani ya sikio ina sehemu mbili:<br>• Koklea: inayohusika na kusikiliza<br>• Mfumo wa vestibula: unapeleka taarifa kwenye ubongo, ambayo inatusaidia kusimama bila kutetereka |  |

### Upotevu wa usikivu ni nini?

Upotevu wa usikivu ni hali inayotokea pale ambapo mtu anakuwa hana usikivu kwa kulinganisha na mtu mwenye usikivu wa kawaida.Anapata taabu kufanya maongezi kwenye mazingira tulivu na  mazingira yenye kelele. Upotevu wa kusikia unaweza kuwa kwa kiwango kidogo hadi kiwango kikubwa.

- Watu wenye upotevu wa kusikia kwa kiwango **kidogo, cha kati au kikubwa** watapata taabu kushiriki kwenye maongezi. Hii inaitwa “kusikia kwa taabu”
- Watu waliopoteza kusikia kwa **kiwango kikubwa** kwa masikio yote mawili huitwa Viziwi

Watu ambao ni viziwi wana mahitaji makubwa na wanapaswa ☞ Kupewa rufaa kwenda kumuona mtaalamu wa masikio na kusikia

Sababu zilizozoeleka zinazasobabisha upotevu wa kusikia ni pamoja na:

- Matatizo yanayotokea kabla,wakati au mara baada ya kuzaliwa
- Kila ugonjwa, kama vile maambukizi ya surua, matumbwitumbwi au maambukizi ya sikio
- Matatizo ya sikio, kama vile kitu kutoka nje ya mwili au sikio lililozibwa kwa nna
- Upotevu wa kusikia unaotokana na umri
- Uharibifu wa kusikia kutokana na kelele kutoka kwenye mazingira yaliyotunzunguka

- Uharibifu wa kusikia kwa sababu ya madawa au kemikali

Uharibifu wa kusikia unaathiri watu katika njia tofauti. Vichanga na watoto wadogo wanahitaji kusikia maongeza ili waweze kupata stadi za kusikiliza na kuongea lugha. Mtu aliyepoteza usikivu anaweza kupata taabu kufuatilia maongezi na taabu akiwa nyumbani, kazini, shuelni na anapokuwa na marafiki. Ni muhimu kubainisha upotevu wa kusikia kwa watoto na watu wazima mapema iwezekanavyo

**Masikio yenye afya bora**

Tunapokagua sikio la mhusika anayepimwa, ni muhimu kuangalia nje na ndani ya masikio; yote ya pande mbili. Hakikisha unakagua sikio kwa mbele na kwa nyuma. Sikio lenye afya njema linapaswa kuwa na:

- Mfereji wa sikio ambao haujazibwa
- Ngoma ya sikio ambayo:
  - Safi (unaweza kuona kwa ndani)
  - Nyeupe/ rangi ya kahawia
- Hakuna dalili ya maumivu wala maambukizi.

Kama pina ya mhusika au mfereji wa sikio haupo au vina umbo la tofauti, mgonjwa atakuwa na mahitaji zaidi na anapaswa ☞ Kupewa rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na kusikia

**Matatizo ya masikio**

Matatizo ya masikio yanaweza kuathiri uwezo wa mtu kusikia. Hata hivyo, matatizo mengi ya usikivu yanaweza kutibika na uwezo wa mtu kusikia unaweza kuwa bora zaidi au kurudi katika hali yake ya awali. Kila mara kagua kujua kama kuna matatizo ya masikio kabla ya kugawa vifaa saidizi vya usikivu kwa mhitaji.

Mtu mwenye matatizo ya masikio anaweza kupata:

- Maumivu
- Kupoteza usikivu
- Kutokwa uchafu kwenye sikio

**Tahadhari!** Maambukizi ya sikio yasipotibika yanaweza kusababisha kupasuka kwa ngoma ya sikio.

Baada ya sababu inayoweza kupelekea upotevu wa usikivu kuondolewa, mgonjwa anaweza kuwa na usikivu vizuri tena. Kila mara hakikisha kuwa mgonjwa ana masikio yenye afya njema na anaendelea kufanya kipimo cha usikivu ili kutathimini kiwango chake cha usikivu.

## Somo la 2: Vifaa saidizi vya usikivu

Vifaa saidizi vya usikivu vinaweza kutumiwa na watu wa umri wote ambao wana shida katika kusikia.

**Vifaa saidizi vya usikivu vinahusisha:**

Vifaa saidizi vya usikivu vilivyozoeleka ni pamoja na:

- **Vifaa saidizi vya usikivu** ni vifaa vya kielektroniki ambavyo vinavaliwa kwenye sikio. Vinaweza kumsaidia mhitaji kwa kuongeza ukubwa wa sauti ili aweze kusikia vyema. Hii ni pamoja na vifaa saidizi livyosetiwa tayari na vile ambavyo vyaweza kusetiwa
- **Mifumo ya spika ndogo binafsi zinaweza kutumika kwa kuendeshwa kwa mbali** zinasaidia watu wanaotumia vifaa saidizi vya usikivu waweze kusikia vyema kwenye maeneo yenye kelele.

**Vifaa saidizi vya usikivu havijajumuishwa**

Vifaa vifuatavyo havijajumuishwa:

- Vifaa saidizi vya usikivu vinavyowekwa ndani ya masikio
- Vipandikizi vya Koklea

- Vitoa ishara ya tahadhari
- Mifumo ya mzunguko
- Mifumo ya usambazaji sauti uwanjani

## Somo la 3: Namna ya kufanya upimaji wa afya ya masikio

Upimaji wa afya ya masikio wa TAP ni mchakato rahisi kujua kama mtoto au mtu mzima ana shida ya masikio na/au anapata shida katika kusikia. Kufanya hivi kunasaidia kubainisha kama mtu anaweza kufaidika na:

- Usafi wa masikio
- Kipimo cha usikivu
- Rufaa kwa mtaalamu wa masikio na usikivu
- Rufaa kwenda kupewa vifaa saidizi

Kabla ya kuanza, andaa nafasi na kufanya kipimo na vifaa. Mwelezee mtu anayepimwa kuhusu upimaji wa afya ya masikio na muombe ruhusa kupima masikio yake.

### Maswali ya upimaji

Muulize mtu anayepimwa maswali ili uweze kujua uzoefu wake na matatizo ya usikivu pamoja na vifaa saidizi vya usikivu.

Baadhi wana mahitaji mengi na watahitaji kupewa ☞ rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu ili waweze kupata tathimini na/ au matibabu. Haya mahitaji yanaweza kuhusisha:

- Watoto walio na umri chini ya miaka mitano.
- Watu wazima na watoto wenye umri wa zaidi ya miaka mitano ambao hawawezi kuzungumza au wale wanaopata shida kuongea.
- Watu wanaotokwa na uchafu mara kwa mara.
- Mabadiliko ya ghafla kwenye kusikia ndani ya muda mfupi ( miezi mitatu)

Kama mhusika tayari anatumia vifaa saidizi vya usikivu, na bado na ana tatizo na vifaa saidizi anavyotumia sasa, kwa ruhusa yake,☞ mpre rufaa kwenye huduma ambayo wanatoa vifaa saidizi.

### Upimaji wa afya ya masikio

Ili kufany aupimaji wa afya ya masikio:

| Hatua | Mambo ya kufanya iwapo sikio lina shida | Mambo ya kufanya iwapo sikio halina shida |
|---|---|---|
| 1. Kagua ndani ya sikio la mgonjwa ( Kuanzia mbele hadi nyuma ya kila upande) | • Kama kuna dalili za:<br>○ **Jeraha, maambukizi** au<br>○ **Kutokuwepo/ umbo tofauti la** sikio/ mfereji wa sikio ☞ Mpe rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu.<br>• Kama mtu ana **jeraha au maambukizi** ⟶ Mwambie arudi ili afanyiwe upimaji wa afya ya masikio baada ya kupata matibabu.<br>• Kama kutakuwepo dalili za **kutokwa na uchafu kwenye sikio** ⟶ Safisha sikio la mgonjwa | Kama **nje ya sikio kuna shida ya kiafya** ⟶ Endelea. Kagua ndani ya sikio la mgonjwa |
| 2. Kagua ndani ya sikio kwa kutumia Otoskopu (kila upande) | • Kama kuna dalili za **maambukizi** ☞ Mpe rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu. Muombe mgonjwa kurudi ili kupimwa tena afya ya masikio baada ya kupata matibabu.<br>• Kama kuna dalili za **tundu kwenye ngoma ya sikio** ☞ Mpe rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu. | If **inside of ear is healthy** ⟶ Plan a hearing test. |

| | | |
|---|---|---|
| | • Kama **sikio limezibwa kwa nnta** au **kuna kitu kutoka nje ya mwili** ⟶ Safisha sikio. Kila mara hakikisha kuwa ni salama kabla ya kuendelea. | |
| 3. Safisha sikio ikiwa itahitajika | • Kama usafi wa sikio **haujafanikiwa** ☞ Mpe rufaa kwa mtaalamu wa masikio na usikivu na muombe kurudi kufanyiwa upimaji wa afya ya masikio kwa mara nyingine baada ya kupewa matibabu. | Kama usafi wa masikio **successful ulifanikiwa** na masikio yana afya njema ⟶ Weka mpango wa kufanya upimaji wa kusikia |

Kama masikio yote yana afya njema ( kwa ndani na kwa nje) weka mpango wa kufanya kipimo cha usikivu ili kutathmini kama mtu anayepimwa anaweza kufaidika na vifaa saidizi vya usikivu

**Namna ya kutumia otoskopu**

- Spekulamu imeambatanishwa kwenye otoskopu. Kifaa hiki kinaingia kwenye mfereji wa sikio wa mtu anayepimwa. Safisha spekulamu kwa kutumia pamba na isafishe kwa kutumia dawa ya kuua wadudu kabla hujaitumia.
- Shika otoskopu kwa mkono wako wa kulia unapokuwa unachunguza sikio la mgojwa la kulia, na tumia mkono wako wa kushoto unapokuwa unachunguza sikio la upande wa kushoto.

**Namna ya kukagua sehemu ya ndani ya sikio.**

1. Osha mikono yako kwa sabuni na ikaishe kila mara kabla na baada ya ukaguzi wa maskio.
2. Angalia kama mgonjwa anasikia maumivu yoyote kwa kubonyeza tragusi. Kama kuna dalili ya maumivu, epuka kutumia otoskopu au itumie taratibu.
3. Kagua kama mgonjwa anatokwa na uchafu. Safisha uchafu kwa kuufuta.
4. Andaa sikio taratibu kwa kuvuta pina kwa juu na kwa nyuma ili kunyoosha mfereji wa sikio. Kwa watoto wadogo vuta pina kwa yuma. Endelea kuvta pina wakati wa otoskopu.
5. Kila mara chomeka otoskopu kwenye sikio la mgonjwa taratibu ili kuepuka kumsababisha maumivu au kumdhuru. Epuka kuchomeka spekulamu kwa ndani sana. Kama mtu anayepimwa atapata maumivu, sitisha upimaji.
6. Kama huwezi kuona mfereji wa sikio, yawezekana ni sababu ya nnta ya sikio inayokuziba usiweze kuona, au, otoskopu haijachomekwa vizuri. Rekebisha namna otoskopu ilivyowekwa kwa ndani kwa kuielekeza kwa juu na kwa mbele ( kuelekea sikio la mhusika)
7. Always check both ears!

**Kufuta uchafu kwenye sikio**

Hii ndio njia salama ya kuondoa uchafu kutoka kwenye sikio la mgonjwa:

1. Osha mikono yako kwa sabuni na ikaushe kabla na baada ya kufuta uchafu kwenye sikio
2. Zungusha kama unakuja sehemu ya mwisho ya tishu ili utengeneza “utambi wa tishu”
3. Vuta pina taratibu juu na kwa nyuma – kwa mtu mzima au kama ni mtoto ivute kwa nyuma.
4. Zungusha taratibu wakati unapochomeka utambi wa tishu sentimita kwa 2-3 kwenye mfereji wa sikio la mgonjwa.
5. Uache utambi kwenye sikio kwa sekunde 10
6. Vuta utambi kwa nje na uangalie kama una usaha au una majimaji mengine.
7. Tupa mbali utambi ambao umeutumia. Zingatia miongozo inayotumika sehemu husika wakati unapotupa tambi zilizotumika.
8. Rudia kwa kutumia utambi mwingine. Endelea kurudia mpaka utambi utakapotoka bila kuwa na maji yoyote.
9. Chunguza ndani ya sikio la mgonjwa kwa kutumia otoskopu ili kuthibitisha kuwa uchafu wote umesafishwa.

**Usafi wa sikio kwa kuoshwa**

Njia hii inatumika kusafisha nnta au kitu kutoka nje ya mwili ; kilichopo kwenye mfereji wa sikio.

**Tahadhari!** Usafi wa sikio kwa kuahsa **haupaswi** kufanyika kama mtu ana:

- Amefanyiwa upasuaji kwa siku za hivi karibuni

- Anajulikana kuwa na tundu kwenye ngoma ya sikio
- Maambukizi ya sikio
- Maumivu ya sikio.

Kama jibu ni ndio kwa mojawapo ya yale yaliyotajwa hapo juu, ☞ mpe rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu.

Ili kusafisha masikio kwa kuosha:

1. Osha mikono kwa sabuni na ikaushe kabla na baada ya kusafisha masikio kwa kuyaosha.
2. Angalia joto la maji. Maji yanapaswa kuwa na uvuguvugu, na yasiwe na joto wala ubaridi. Jaza bomba la sindano kwa mililita 20 za maji.
3. Muombe mgonjwa kushikilia kifaa cha kuweka uchafu chenye umbo la figo, au bakuli; chini ya sikio huku akibana kifaa hicho kwenye ngozi ya shingo.
4. Weka mdomo wa bomba la sindano kwenye mfereji wa sikio la mgonjwa
5. Weka bomba la sindano likielekea upande wa juu wa mfereji wa sikio na taratibu kuelekea nyuma.
6. Bana bomba la sindano ili kusukuma maji kwenye mfereji wa sikio la mgonjwa.
7. Maji yatamwagika kwenye bakuli na yanaweza kuwa na nnta au kitu kutoka nje ya mwili.
8. Kagua sikio la mgonjwa kwa mara nyingine kwa kutumia otoskopu
9. Rudia kusafisha sikio kwa maji kama itahitajika kusafirisha sikio lililozibwa
10. Kagua sikio la mgonjwa kila baada ya kusafisha sikio kwa kuliosha.

**Tahadhari !** Acha kusafisha sikio kwa kuliosha kama mgonjwa atahisi maumivu ya sikio.

Kama sikio la mgonwa litaendelea kuwa limezibwa baada ya kujaribisha kulisafisha mara tatu, muombe arudi tena siku inayofuata na rudia kulisafisha kwa kuliosha. Kama nnta hataondolewa yote baada ya kuja hospitali mbara mbili. Kwa ruhusa ya mgonjwa, ☞ Mpe rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu.

## Somo la 4: Weka mpango

### Vifaa saidizi vingine

Wakati wa upimaji wa afya ya sikio, muulize kama mgonjwa ana shida kwenye maeneo mengine. Kwa mfano, uoni, uwezo wa kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, kujitunza, mawasiliano au utambuzi ) kufikiria na/au kukumbuka)

### Hatua zinazofuata

- **Kupima:** Kama mtu anayepimwa ana shida maeneo mengine muulize kama angependa kupimwa kwenye tatizo linalomsumbua.
- **Kutathmini:** Kama mtu anayepimwa ana masiko yenye afya bora, fikiria kumpima usikivu.
- **Ktoa rufaa:** Utoaji rufaa unapaswa kujadiliwa na kukubaliana na mgonjwa.
- **Kufuatilia:** Ni muhimu kuweka miadi ya kufuatilia ili kupima masikio kwa mara nyingine baada ya matibabu ya maambukizi ya masikio ☞ Mpe rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu.